PDPC FARAGHA NEWSLETTER
Toleo Na. 0006 Aprili - June 2026




# KONGAMANO LA KWANZA LA MWAKA

## LA FARAGHA NA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI, TANZANIA: *LILIFANA NA KUACHA ALAMA.*

## **MKURUGENZI MKUU PDPC:** USAJILI WA LAZIMA WAANZA, HATUA ZA KISHERIA KUCHUKULIWA.

Taasisi zote zinapaswa kujiandaa kwa Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPA). **UK. 06**

# YALIYOMO

03 KONGAMANO LA KWANZA LA MWAKA LA FARAGHA NA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI, TANZANIA: LILIFANA NA KUACHA ALAMA.

06 MKURUGENZI MKUU PDPC: USAJILI WA LAZIMA WAANZA, HATUA ZA KISHERIA DHIDI YA WANAOKIUKA SHERIA KUCHUKULIWA.

08 PDPC NI MHIMILI MUHIMU MUSTAKABALI WA TANZANIA YA KIDIJITALI

09 HABARI PICHA.

12 MATANGAZO.

14 WAKAZI WA DODOMA WAKOSHWA NA PDPC: MAONESHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA - 2026.






# KONGAMANO LA KWANZA LA FARAGHA NA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI TANZANIA: LILIFANA NA KUACHA HISTORIA

Kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Angella Jasmine Mbellwa Kairuki (Mb), Juni 29, 2026 Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Dkt. Switbert Zacharia Mkama (Mb) alifungua rasmi Kongamano la Kwanza la Kitaifa la Faragha na Ulinzi wa Taarifa Binafsi la mwaka 2026.

Akifungua kongamano hilo, Mhe. Mkama alisema kuwa uchumi wa kidigitali tunaoutamani hauwezi kujengwa juu ya teknolojia pekee bali unahitaji kuaminiana kati ya wananchi, Serikali, taasisi za umma na sekta binafsi kupitia mfumo madhubuti wa Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

“Ni vyema kuwa na kongamano rasmi la masuala ya Faragha na Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa lengo la kukutana kwa pamoja na kujadiliana maswala muhimu yanayohusu Faragha na Ulinzi wa Taarifa Binafsi na kuwa na mwelekeo wa pamoja kama taifa” alisema Mhe. Dkt. Mkama.

“Kwa sasa huduma nyingi za Serikali na taasisi binafsi zinatolewa kupitia mifumo ya TEHAMA na kumekuwa na jitihada za kuhakikisha mifumo hiyo inasomana na kubadilishana taarifa. Ni vyema mifumo hiyo inapobadilishana taarifa izingatie misingi ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi inayokubalika kitaifa, kikanda na kimataifa na hivyo imani ya wawekezaji wa ndani na nje ya nchi itaongezeka” aliongezea Mhe. Dkt. Mkama

Mhe. Dkt. Mkama pia aliipongeza kwa dhati bodi na menejimenti ya PDPC kwa kuandaa kongamano hilo na kusema kuwa kongamano hilo limekusudia kuifanya Tanzania kuwa jukwaa la kitaifa na kikanda la kubadilishana uzoefu, kujifunza na kujenga ushirikiano wa Faragha na Ulinzi wa Taarifa Binafsi.

PDPC ni taasisi muhimu ya kujenga imani ya wananchi katika Uchumi wa kidigitali kwa kuhakikisha uzingatiaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa taasisi za umma na binafsi unaonwa kama sehemu ya kujenga Imani ya wananchi kwao kwa kuhakikisha zinawekeza katika mifumo salama ya usimamizi wa taarifa na kujenga uwezo wa watumishi wao.








Baadhi ya Wadhamini wa Kongamano la Kwanza la Mwaka la Faragha na Ulinzi wa Taarifa Binafsi Tanzania, wakipokea Tunzo maalumu kutoka kwa Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu, Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (WMTH), **Bi. Fatuma Zuberi Kalovya,** aliekuwa Mgeni Rasmi kwenye Hafla ya kufunga Kongamano hilo, Julai 01, 2026.










Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia akizungumza na Waandishi wa Habari (Hawapo pichani) kwenye Mkutano na Waandishi wa Habari uliofanyika June 12, 2026 jijini Dodoma.

# **MKURUGENZI MKUU PDPC:** USAJILI WA LAZIMA WAANZA, HATUA ZA KISHERIA DHIDI YA WANAOKIUKA SHERIA KUCHUKULIWA.

Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), Dkt. Emmanuel Mkilia, Juni 12, 2026 ametoa wito kwa taasisi zote zinazokusanya au kuchakata Taarifa Binafsi kuhakikisha zinazingatia matakwa ya Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44, huku akisisitiza kuwa utekelezaji kamili wa Sheria hiyo umeanza na hatua za kisheria dhidi ya wanaokiuka masharti yake zinaendelea kuchukuliwa.

Dkt. Mkilia alisema hatua hizo zimeanza tangu Aprili 9, 2026 baada ya kukamilika kwa kipindi cha usajili wa hiari tarehe Aprili 8, 2026.

Kwa mujibu wa Sheria hiyo, ni marufuku kwa taasisi yoyote kukusanya au kuchakata Taarifa Binafsi bila kusajiliwa na Tume kama Mkusanyaji na/au Mchakataji wa Taarifa Binafsi. Taasisi zitakazobainika kufanya shughuli hizo bila usajili zitakuwa zinatenda kosa la kisheria na zinaweza kuchukuliwa hatua mbalimbali za kisheria na kiutawala, ikiwemo kutozwa faini kwa mujibu wa Sheria.

“Mpaka Aprili 8, 2026, zaidi ya taasisi 14,000 zilikuwa zimejisajili. Huu ni mwitikio mzuri unaoonesha dhamira ya wadau katika kulinda faragha na taarifa binafsi za wananchi,” alisema.

Aidha, alitoa maelekezo kwa taasisi ambazo bado hazijakamilisha au kuanza mchakato wa usajili kuhakikisha zinakamilisha taratibu hizo ndani ya siku saba za kazi kuanzia Juni 12, 2026.

Aliongeza kuwa taasisi zote zinapaswa kujiandaa kwa ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria ambao tayari umeanza, pamoja na kuhakikisha zinakuwa na sera zilizoidhinishwa za Ulinzi wa Taarifa Binafsi na mifumo madhubuti ya kulinda Taarifa hizo.

Wakati huo huo, Dkt. Mkilia aliwaalika wadau mbalimbali kujiandikisha na kushiriki Kongamano la Kwanza la Taifa la Faragha na Ulinzi wa Taarifa Binafsi litakalofanyika kuanzia Juni 29 hadi Julai 01, 2026 katika Ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam.

Alisema kongamano hilo litawakutanisha wataalamu, watunga sera, wasimamizi wa Sheria, sekta binafsi, watafiti na wadau wengine kutoka ndani na nje ya nchi kujadili masuala ya Faragha, Ulinzi wa Taarifa Binafsi na mustakabali wa huduma za kidijitali Nchini.








# PDPC NI MHIMILI MUHIMU MUSTAKABALI WA TANZANIA YA KIDIJITALI

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) imetajwa kuwa taasisi muhimu katika kujenga mustakabali wa Tanzania ya kidijitali kupitia kuimarisha uaminifu, usalama wa mtandao, ubunifu na biashara ya kidijitali.

Hayo yalielezwa Juni 16, 2026 katika Kongamano la Afrika la Ubunifu na Teknolojia (Africa Innovation Technology Forum 2026) lililofanyika jijini Dar es Salaam na kuwakutanisha watunga sera, wadhibiti, wataalamu wa teknolojia na viongozi wa sekta mbalimbali kujadili fursa na changamoto za maendeleo ya kidijitali barani Afrika.

Akizungumza kama mchangia mada katika mjadala uliohusu Ujenzi wa Mfumo Jumuishi wa Kitaifa wa Utawala wa Kidijitali: Kuoanisha Udhibiti wa TEHAMA, Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Usalama wa Mtandao, Ubunifu na Sera za Biashara kwa Ukuaji Endelevu, Mkuu wa Kitengo cha Sheria wa PDPC, Wakili Humphrey Mtuy, alisema jukumu la Tume halijikiti tu katika kulinda haki za faragha, bali pia katika kusaidia ujenzi wa mfumo madhubuti wa utawala wa kidijitali unaojumuisha sekta zote muhimu za uchumi wa kidijitali.

Alisema kuwa kadri Tanzania inavyoendelea kutekeleza ajenda yake ya mabadiliko ya kidijitali, PDPC ina nafasi ya msingi katika kuhakikisha maendeleo hayo yanazingatia haki za faragha za watu, yanakuwa jumuishi na yanajenga mazingira salama ya ukuaji wa uchumi.

“Utawala bora wa taarifa binafsi hujenga uaminifu unaohitajika kwa ajili ya ubunifu, uwekezaji na ukuaji endelevu wa uchumi. Pia huongeza imani ya wananchi katika matumizi ya huduma za kidijitali na kuwezesha mtiririko salama wa taarifa unaochochea biashara ya kidijitali ndani na nje ya nchi,” alisema Wakili Mtuy.



**HABARI PICHA**

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) imetoa mafunzo ya dhana ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi kwa Kanisa katoliki na mashirika yake nchini zikiwemo shule, hospitali, vituo vya kulelea Watoto yatima, wagonjwa na huduma nyingine za kijamii.

Mafunzo hayo yalifunguliwa na Katibu Mkuu wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC) Padri Dkt. Charles Kitima.










**HABARI PICHA**

Watumishi wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC), tarehe 1 Mei 2026 tuliungana na wafanyakazi wote Nchini kusheherekea siku ya wafanyakazi duniani (Meimosi). Tulisheherekea siku hii, tukitambua mchango wa kila mmoja katika kuimarisha Ulinzi wa Taarifa Binafsi Nchini.

Maadhimisho hayo yaliambatana na Kauli Mbiu isemayo "Kazi zenye staha ni nguzo imara kwa maendeleo endelevu katika utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050".




PDPC
MEI MOSI - 2026
Kauli Mbiu:
"Kazi zenye Staha ni Nguzo Imara kwa Maendeleo Endelevu
katika Utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050"
FARAGHA YAKO NI WAJIBU WETU







JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

# TAARIFA KWA UMMA

## KUHUSU UTEKELEZAJI NA UZINGATIAJI WA SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI, SURA YA 44

**Dodoma – Juni 12, 2026.**

Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) inapenda kuutaarifu umma, wakusanyaji na wachakataji wa taarifa binafsi kwamba utekelezaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi, Sura ya 44, sasa umeanza kutumika kikamilifu na uchukuaji wa hatua za kisheria kwa wanaokiuka matakwa ya Sheria tajwa kuanzia tarehe 9 Aprili, 2026, kufuatia kukamilika kwa kipindi cha usajili wa hiari tarehe 8 Aprili, 2026.

Kwa mujibu wa Sheria hiyo, ni marufuku kwa taasisi yoyote kukusanya au kuchakata taarifa binafsi bila kusajiliwa na Tume kama Mkusanyaji au/na Mchakataji wa Taarifa Binafsi. Taasisi yoyote itakayobainika kukusanya au kuchakata taarifa binafsi nchini bila usajili inatenda kosa la kisheria na itachukuliwa hatua kali za kisheria, ikiwa ni pamoja na adhabu ya kupigwa faini au kuchukuliwa hatua za kiutawala kama zilivyoainishwa kwenye Sheria.

Tume inazitambua na kuzipongeza taasisi zote zilizokamilisha usajili wao ndani ya kipindi cha hiari. Kufikia tarehe 8 Aprili, 2026, zaidi ya taasisi 14,000 zilikuwa zimejisajili, hatua inayoonesha mwitikio chanya wa wadau katika kulinda faragha na taarifa binafsi za wananchi. Taasisi hizi zinatakiwa kuendelea kuzingatia kikamilifu matakwa ya Sheria, ikiwa ni pamoja na kuwa na sera za ulinzi wa taarifa binafsi na kuhakikisha mifumo yao inalinda taarifa dhidi ya matumizi yasiyoidhinishwa.

Hata hivyo, Tume imebaini kuwa bado kuna taasisi kadhaa zinaendelea kukusanya na kuchakata taarifa binafsi bila kuzingatia matakwa ya Sheria, hususan katika Sekta nyeti kama Afya na Elimu. Hali hii ni ukiukwaji wa moja kwa moja wa Sheria na inaleta hatari kwa haki za msingi za faragha za wananchi.

Kutokana na hali hiyo, Tume inatoa maelekezo yafuatayo:

**1.** Taasisi zote ambazo zilianza mchakato wa usajili lakini hazijakamilisha zinatakiwa kukamilisha ndani ya siku saba (7) za kazi kuanzia leo tarehe 12/06/2026;

**2.** Taasisi ambazo hazijaanza kabisa usajili zinatakiwa kuanza na kukamilisha ndani ya siku saba (7) za kazi kuanzia leo tarehe 12/06/2026;

UK. 1

Mtaa wa Moshi 1, Viwandani, S. L.P 1105, 41102 Dodoma - Tanzania
Simu: +255718462536, +255744057652, +255736110505.
@pdpc.tz @pdpc_tz www.pdpc.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

# TAARIFA KWA UMMA

**3.**Taasisi zote zinatakiwa kujiandaa kwa ukaguzi wa uzingatiaji wa Sheria ambao umekwishaanza na unaendelea; na

**4.**Taasisi zote zinapaswa kuhakikisha zina sera zilizoidhinishwa za ulinzi wa taarifa binafsi na mifumo madhubuti ya ulinzi wa taarifa.

Tume inawakumbusha wananchi kuwa wana haki ya kulinda taarifa zao binafsi kwa mujibu wa Sheria. Wananchi wanahimizwa kutumia haki zao, ikiwemo kuwasilisha malalamiko Tume endapo watabaini matumizi yasiyo halali ya taarifa zao au ukiukwaji wa faragha zao.

Tume itaendelea kutoa elimu, miongozo na usimamizi ili kuhakikisha Tanzania inakuwa na mfumo imara wa ulinzi wa taarifa binafsi unaolinda haki za wananchi na kuimarisha imani katika matumizi ya teknolojia na huduma za kidijitali. Kwa kuzingatia umuhimu wa elimu kwa umma, Tume imepanga kufanya Kongamano la Kwanza la Faragha na Ulinzi wa Taarifa binafsi kuanzia tarehe 29 Juni hadi tarehe 1 Julai, 2026 Jijini Dar es Salaam katika Ukumbi wa Mlimani City.

Maafisa Ulinzi wa Taarifa Binafsi na timu zao za Faragha katika kila taasisi wanashauriwa kushiriki Kongamano hili muhimu kwa ajili ya kujenga uelewa na kushiriki majadiliano na kujifunza kutoka kwa wadau mbalimbali wa Faragha na Ulinzi wa Taarifa Binafsi kutoka nchi mbalimbali duniani. Kongamano hili ni jukwaa mahsusi la kubadilishana maarifa, kujadiliana masuala ya teknolojia zinazoibukia, kubadilishana uzoefu na kuimarisha ushirikiano hususan katika uhamasishaji wa huduma za kidijitali salama, zinazoaminika na jumuishi zinazoshabihiana na Dira ya Taifa 2050.

**Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana nasi:**
Simu: +255753459155, +255718462536, +255744057652, +255736110505, na +255615779070 au Baruapepe: helpdesk@pdpc.go.tz

**Imetolewa na:**
**Dkt. Emmanuel Lameck Mkilia**
**Mkurugenzi Mkuu - PDPC**

*"FARAGHA YAKO NI WAJIBU WETU"*

UK.2

Mtaa wa Moshi 1, Viwandani, S. L.P 1105, 41102 Dodoma - Tanzania
Simu: +255718462536, +255744057652, +255736110505.
@pdpc.tz @pdpc_tz www.pdpc.go.tz



# WAKAZI WA DODOMA WAKOSHWA NA PDPC: MAONESHO YA WIKI YA UTUMISHI WA UMMA - 2026.

Wakazi mbalimbali wa Jiji la Dodoma walitembelea banda la Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) na kujifunza kazi na majukumu mbalimbali yanayotekelezwa na PDPC kwenye Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, 2026 yaliyofanyika jijini Dodoma.

Akizungumza mara baada ya kutembelea banda la PDPC na kupatiwa elimu kuhusu Tume inavyotekeleza majukumu yake, Bw. Victor John, alisema ameridhishwa na huduma zinazotolewa na PDPC na jinsi huduma hizo zinavyokuwa msaada kwa wananchi.

"Kwa kweli, hii Taasisi imekuja wakati muafaka wa kidigitali na nimeridhishwa na PDPC kwa huduma nzuri wanayotoa katika maonesho haya kwani nimepokelewa vizuri na kujifunza mengi kuhusu Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi Pia, huduma za kusajili taasisi zinazokusanya na kuchakata Taarifa na kupata vyeti kwa urahisi kupitia mfumo," alisema Bw. John.

Aidha Bw. John alitoa ushauri kwa Tume kuweka nguvu kubwa kwenye Elimu kwa Umma na kuongeza ofisi kwaajili ya kutoa huduma kwenye mikoa.

"Nashauri hii Tume iweke nguvu kwenye kujitangaza kwakua ni mpya watu wengi hawaifahamu hivyo itakua vema ikiweka nguvu kwenye kuelimisha watanzania kuhusu uwepo wa Tume hii na ikiwezekana wafungue matawi kila mkoa" alisema Bw. John

Katika maonesho ya wiki ya Utumishi wa Umma, wananchi wanapata fursa ya kujifunza masuala mbalimbali yahusuyo PDPC ikiwemo Majukumu ya Tume na namna ya kuutumia mfumo wa Usajili na Malamiko.





Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu (DAHRM), Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, **Bi. Fatuma Zuberi Kalovya**, tarehe 17 Juni 2026, alitembelea banda la Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) ikiwa ni siku ya pili ya Maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika katika Viwanja wa Chinangali Park jijini Dodoma.











Ni baadhi ya wakazi wa Jiji la Dodoma waliotembelea banda la Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC) na kujifunza kazi na majukumu yanayotekelezwa na PDPC wakipokea zawadi ya Vipeperushi kutoka kwa Maafisa Rasilimaliwatu (HR) wa PDPC katika Maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma, 2026 yaliyofanyika kwenye Viwanja vya Chinangali Park, jijini Dodoma kuanzia Juni 16 mpaka Juni 23, 2026.






TUME YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

# Karibu kwenye Ukurasa Rasmi wa **LinkedIn** wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi,Nchini Tanzania (PDPC)

Kadiri Tanzania inavyopiga hatua katika mabadiliko ya kidijitali, uvumbuzi na uchumi wa kidijitali, Ulinzi wa Taarifa Binafsi na haki za faragha unasalia kuwa kipaumbele cha kitaifa.

**Jukwaa hili litatumika kama njia ya:**

- Kushirikisha wadau
- Matangazo na mipango ya taasisi
- Kuelimisha na kuongeza uelewa wa umma
- Kutoa maarifa kuhusu Ulinzi wa Taarifa Binafsi
- Kutoa Taarifa mpya za kikanuni na mwongozo wa Uzingatiaji wa Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi

Tunaendelea kujitolea kukuza ushughulikiaji wa Taarifa Binafsi Nchini Tanzania ambao ni halali, salama, wa wazi na unaozingatia uwajibikaji.

Kwa pamoja, tunajenga mustakabali wa kidijitali Nchini

Jiunge nasi Kwenye

**LinkedIn**

@pdpc.tz






**HABARI PICHA**

Ni baadhi ya washiriki wa Kongamano la Kwanza la Mwaka la Faragha na Ulinzi wa Taarifa Binafsi kutoka ndani na nje ya nchi wakifatilia Mada mbalimbali zilizotolewa kwenye kongamano hilo lililofanyika jijini Dar es salaam kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNICC) kuanzia  Juni 29 mpaka Julai 1, 2026.




















**Huduma kwa wateja:**


Simu:

**+255753459155**
**+255718462536**
**+255744057652**
**+255615779070**
**+255736110505**

Barua pepe:

**helpdesk@pdpc.go.tz**

Mkurugenzi Mkuu,
Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi,
S.L.P 1105, 1 Mtaa wa Moshi,
Viwandani, 41102 Dodoma.